

**MKINGA DISTRICT COUNCIL  
GOMBERO SECONDARY SCHOOL  
P.O BOX 2157, TANGA.**

TAREHE.....

**Ref. No. GSS/K.1/014/VOL.1/04**

JINA LA MWANAFUNZI.....  
SHULE YA MSINGI ATOKAYO.....

**MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GOMB ERO MWAKA 2018**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Gombero, hongera sana kwa kufaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na kupata nafasi ya kujinga na shule ya sekondari Gombero.

Ni mategemeo yangu kuwa utatumia nafasi hii vizuri mpaka utakapo maliza kiwango hiki cha elimu ya sekondari, ili hatimae utoe mchango wako katika ujenzi wa taifa.

Wanafunzi wa kidato cha kwanza wafike shulenii kuanzia tarehe **8.01.2018 MWISHO Tarehe 15.01.2018**.shule hii ni ya kutwa na yenye mchanganyiko ya wanafunzi wa kike na wa kiume, ipo umbali wa kilometra 29 kutoka Tanga mjini na meta 400 kutoka barabara kuu ya Maramba – Tanga. Kikao cha wazazi wenye watoto waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kitafanyika siku **ALHAMISI** tarehe **28.12.2017** Tafadhalii fika bila kukosa. Kikao kitaanza saa 3 asubuhi.

Pamoja na barua hii naambatanisha :-

1. Orodha ya mahitaji muhimu ya shule
2. Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi
3. Fomu ya hospitalini
4. Kanuni na sheria za shule
5. Fomu ya kukubali nafasi uliyopewa

Fomu ya hospitali ijjazwe na daktari katika hospitali ya serikali. Mwanafunzi aje na fomu zote zikiwa zimejazwa kikamilifu siku ya kufungua shule bila kukosa na azikabidhi kwa mkuu wa shule ndio atapata usajili.

Karibu sana Gombero Sekondari

**ATHUMANI MRISHO ABDALLAH  
MKUU WA SHULE**

Nakala:-

1. Katibu mkuu,  
Wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi  
SLP 9121  
DAR ES SALAAM

2. Mkaguzi Mkuu wa shule kanda,  
Kanda ya kaskazini Mashariki,  
SLP 460  
MOSHI

3. Afisa Elimu mkoa,  
SLP 313,  
TANGA.

4. Afisa Elimu sekondari,  
Wilaya ya Mkinga,  
SLP 6005,  
TANGA.

## **ORODHA YA MAHITAJI YA MWANAFUNZI**

### **1. VIFAA VYA DARASANI**

- Madaftari 13, peni, penseli na mkebe
- Kamusi (dictionary)
- Vitabu mbalimbali

### **2. SARE ZA SHULE**

#### i. Wavulana

- ✓ Suruali mbili za kijani (Ona mfano wa kitambaa)na mashati mawili meupe yenyenye mikono mifupi
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba. Raba haziruhusiwi.

#### ii. Wasichana

- ✓ Sketi mbili za kijani (ona mfano wa kitambaa). Urefu ufile kwenye kongo za miguu na si magotii.
- ✓ Kwa wanafunzi wa kiislamu, Hijabu ni sketi mbili ndefu zifike kwenye kongo za miguu. Nusu kanzu mbili zinazofika kwenye magotii.
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba. Bajaji haziruhusiwi.

#### iii. Nguo za michezo na raba

iv. Tai ya kijani nzuri na ya heshima na ifanane na sketi/ suruali ya wanafunzi.

### **3. VIFAA VINGINE**

- ✓ Wanafunzi aje na cheti halasi cha kuzaliwa

## **SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Mwanafunzi anapaswa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na shule kwani ndio dira na usalama wake awapo shulenii.

### **A. SHERIA ZA NCHI**

Kila wanafunzi anawajibika kutii na kufuata sheria zote za nchi.

### **B. MASOMO**

Kila wanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule kama ilivyopangwa na ikiwemo kuwahi shulenii na kubaki shule hadi mwisho wa viupindi. Masomo yafundishwayo hapa shulenii ni Civics, Physics, Chemistry, Biology, Geography, Elimu ya dini ya kiislamu, Kiswahili, Basic Mathematics, History, English language na kiarabu.

## C. MAADILI

- i. **HESHIMA**- Mwanafunzi anapaswa awaheshimu walimu,wafanyakazi,wasio walimu, viranja, wanafunzi wenzake na wananchi ndani na nje ya mazingira ya shule.
- ii. **USAIFI**- Kila mwanafunzi hana budi kuzingatia usafi wa mwili,mavazi na mazingira wakati wote akiwa mazingira ya shule na nje ya shule.
- iii. **MWANAFUNZI HATAKIWI KUFANYA YAFUATAYO.**  
-Kuvuta sigara, Bangi, kutumia madawa ya kulevyaa au kunywa pombe  
-Kutembelea vilabu nya pombe , nyumba za starehe au nyumba za kufikia wageni (guest house)  
-Kutumia lugha mbaya na za kihuni kwa wanafunzi wenzake, walimu na watu wengine.
- iv. Ni marufuku kujiipamba mfano: kutia dawanywele,kupaka rangi kwenye kucha, midomo, kujichubua ngozi kwa dawa, kuvalaa herein, pete au bangili, kuvalaa mikanda mipana, kuandika maandishi kwenye mwili, pia hairusiwi kunyaa mitindo ya kihuni.
- v. Wanafunzi watavaa sare wakati wa
  - a. Masmo darasani
  - b. Wanapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
  - c. Wanapokwenda hospitalini.

## D. LUGHA.

Masomo yote isipokuwa KISWAHILI,ELIMU YA DINI YA KIISLAMU na KIARABU yatafundishwa kwa lugha ya kiingereza.Tunasisitiza kuwa lugha rasmi ya mawasiliano hapa shulenii ni KIINGEREZA.

## E. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa
4. Uvutaji wa bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga au kupigana
7. Kudharau bendera ya taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kuharibu mali ya uma kwa makusudi
10. Kupata mimba au kumpa msichana mimba
11. Kugoma,kuchochea au kuongoza mgomo/vurugu.

